**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MJI WA TARIME**

**Shule ya Sekondari Tarime**

**S.L.P 183,**
**TARIME.**

**KUMB.NA. THS/JI/F5.2026/Vol.1/…..** **13/05/2026.**

**Namba za simu :**
**Mkuu wa shule: 0756321224/0785321224**
**Makamu mkuu wa shule: 0752233880AU 0718406330**
*Namba za kutuma pesa kwa mwanafunzi Shuleni:* ***0793466166/0680967086(JINA: Tarime Sec School)***

**MZAZI/MLEZI wa Mwanafunzi …………………….**
**S.L.P……….............................**
**……………………………………..**

**YAH:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA ***TANO*** KATIKA ***SHULE YA SEKONDARI TARIME*** HALMASHAURI YA ***MJI TARIME*** MKOA ***MARA*** MWAKA **.............................**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha ***TANO*** katika shule ya ***Sekondari Tarime*** mwaka…………….Tahasusi y ………………..…….**hongera sana!!!**

2. Shule hii ni ya Bweni ipo umbali wa kilometa **2½** kutoka Tarime Mjini.Ukiwa Unatokea Mwanza shuka kituo kinachoitwa **BUHEMBA.** Kutoka Buhemba hadi shule ni **mita 200 hauhitaji usafiri wowote, ukishukia stendi kuu ya mabasi mjini** nauli ni Shilingi ***2,000/=*** kwa pikipiki na Shilingi ***1,000/=*** kwa bajaji.

3. Muhula wa Masomo unaanza tarehe **.....................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **...................**Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………………….**

## A. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 1.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule ni **SURUALI NYEUSI NA SHATI NYEUPE**.
ii. Suruali mbili nyeusi pana mapajani zenye marinda mawili pande zote, mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele) yenye upana wa inch 18 miguuni.
iii. Shati mbili (02) nyeupe za mikono mirefu na zenye mfuko mmoja tu.
iv. Tai Nyeusi
v. Viatu vya shule ni vya **NGOZI**vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;***( UNAWEZA PIA KUVIPATA DUKA LA SHULE)***
vi. Soksi nyeusi jozi mbili (02) na zisiwe na mistari au madoadoa.
vii. Sweta rangi ya**ke kama inavyoonekana kwenye picha** (V – Shingoni**ISIYO NA MFUKO**).**( Unaweza pia kuipata shuleni ikiwa na nembo ya shule kwa watakaohitaji)**



viii. Sare ya michezo ( JEZIna Bukta ya Bluu).



**( Unaweza pia kuipata shuleni ikiwa na nembo ya shule)**

ix. T-shirt mbili rangi ya **PINK POLLO T-SHIRT- yenye kola**, **isiyo na mfuko-** (**( Unaweza pia kuipata shuleni ikiwa na nembo ya shule)**



x. Tracksuit kama inavyoonekana kwenye picha **( Unaweza pia kuipata shuleni ikiwa na nembo ya shule)**



xi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

**xii.** Nguo za kushindia;Surua 2 za ***KHAKI*** **(ESTEM Na.1**) pana mapajani yenye marinda mawili pande zote, mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele) yenye upana wa inch 18 miguuni pamoja .

**xiii. Kwa wanafunzi wote wa masomo ya sayansi kwa vitendo lazima aje LAB COAT (anaweza pia kuipata shuleni ikiwa na muhuri wa shule). Tahasusi husika ni PCM, PCB, CBG na PMC. Ni vazi rasmi wakati wa mazoezi na mitihani kwa vitendo.**

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari (QUIRE 3 AU 4 =*12*);
ii. **Ream (A4)** Mbili (2)
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
**iv. Scientific Calculator;**
**v. Fedha ya walimu wa kujitolea, motisha kwa walimu Tshs. 60,000/= kwa mwaka kwa makubaliano ya wazazi na kibali cha mkuu wa wilaya.**
vi. Godoro la sponge(***Vita form/Tan form/Super Banco/ Dulax*** n.k): upana wa ft 2½ (sm 75) x 6''
vii. Mashuka Jozi 2(Pink/Bluu bahari), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 Mto 1, Taulo
viii. Nguo za ndani za kutosha, Ndala/kandambili za kuogea
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko; na Dumu la lita tano la kutunzia maji ya kunywa
xi. Vifaa vya usafi ambavyo mwanafunzi anatikiwa kuja navyo kama vinavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

| **Na** | **Tahasusi** | **Aina ya vifaa anavyotakiwa kuwasilisha** |
|---|---|---|
| 1. | PCM | Kwanja, hardbroom, mopa na ndoo yake, chelewa |
| 2. | PCB | Jembe, chelewa na mkasi wa kukatia maua na kwanja na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 |
| 3. | CBG | Reki,squizer, na Brashi ya kusafishia choo na chelewa |
| 4. | PMC | Softbroom,mopa na ndoo yake, Dawa **ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 na chelewa** |
| 5. | **HGK** | Squizer 1, Mopa na ndoo yake 1, mkasi wa kukatia maua 1, na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 |
| 6. | **HGL** | Brashi ya kusafishia choo 1, Mopa na ndoo yake 1, jembe 1, na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita |
| 7. | **HKL** | Kwanja 1, jembe 1, reki 1 na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 |
| 8. | **EGM** | Softbroom 1, hardbroom 1, Chelewa 1, na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 |
| 9. | **HGE** | Softbroom 1, hardbroom 1, Chelewa 1, na dawa ya chooni aina ya Spark Kleen lita 5 |

**xii.** Sanduku la bati kwa kutunzia vitu vyake **(ni lazima).Mabegi na masanduku ya thamani kubwa hayatakiwi shuleni.**

**MUHIMU:** ***MAHITAJI YOTE HAYO YANAPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE. HIVYO KUEPUKA USUMBUFU WA KUSAFIRI NA MIZIGO UNASHAURIWA KUCHUKULIA MAHITAJI HAYO SHULENI. GHARAMA NI ZILEZILE ZA SOKONI.***

**1.2 Michango mbalimbali ya Shule**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha iwekwe Kwenye ***A/C NO. 30401200086 NMB*** Jina la akaunti ni **TARIME SECONDARY SCHOOL (DEVELOPMENT A/C).**Mwanafunzi afike na bank pay inslip yenye jina lake kurahisisha kazi za uhasibu hasa ukataji wa stakabadhi. **Mwanafunzi asije na pesa taslimu mkononi siku ya kuripoti.**

## MUHIMU SANA.

**BIMA YA AFYA:**

**Kila mwanafunzi kwa kujali afya yake anapaswa kuja na kadi ya bima ya afya iliyo hai. Hivyo kila mwanafunzi** aje nayo kwa matumizi yeke binafsi. Shule huwa inapata wakati mgumu sana kumhudumia mwanafunzi asiye na bima na wanafunzi wengi wamekuwa wakirudishwa nyumbani kufuata matibabu au wazazi kutumia gharama kubwa kutuma pesa za matibabu.***MUHIMU SANA:MWANAFUNZI AJE NA NAMBA YA NIDA ILI KUFUNGUA KADI YA BIMA. MWANAFUNZI AJE NA KITAMBULISHO CHA TAIFA AU NAMBA YA NIDA. ILI KUMSAJILI APATE NHIF CARD. Kwa mwanafunzi asiye na Bima ya afya aje na pesa taslimu kiasi cha Tshs 50,400/=***

## B. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

1. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
3. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa). MUHIMU.
4. Siku ya kuja shuleni kuanza masomo Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare ya shule vinginevyo hata pokelewa (shati nyeupe na suruali nyeusi na tai).
5. Nguo zote za kiraia haziruhusiwi kabisa kuonekana wala kuvaliwa shuleni, hivyo basi mwanafunzi asije nazo shuleni kabisa.

6. Mzazi/mlezi hakikisha mwanao anapimwa afya yake kikamilifu katika hospitali ya serikali na siyo vinginevyo. Ukifanya udanganyifu hatutakubali sababu zozote zitakazotolewa baadaye. Shule tumebaini kuna baadhi ya wanafunzi hawapimwi kabisa afya zao, badala yake fomu hujazwa bila kufanyiwa vipimo, anapofika shuleni huugua huku fomu inaonesha hana tatizo lolote la kiafya.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## C. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;(**Mzazi hakikisha kweli mwanao anapimwa afya yake**)
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
vi. Aje na results slip ’’**original**’’

**D.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**




**<u>CHENGE J.M</u>**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha

kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule : 0756321224/0785321224: Makamu Mkuu wa Shule:**0752233880AU 0718406330**
- Mwandamizi Taaluma:0768 427 232; MwalimuMalezi wa Bweni (Boarding Master) :0762922400

**Mzazi/mlezi** kumbuka kwamba, ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Unaombwa/ Unashauriwa na **BODI** ya shule kumnunulia mwanaoangalau kitabu kimoja kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma **(Vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni)**.

| NA | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| 1. | Biology | 1. Biology for Form Five TIE<br>2. New understanding Biology for Advanced level By Suzanne Toole, Complete advanced Biology by Respicious R<br>3. 2. Biological Science By Taylor DJ, Adv. Manual |
| 2. | Chemistry | 1. Physical Chemistry TIE<br>2. Organic Chemistry TIE<br>3. General Chemistry TIE. |
| 3. | Advanced Maths | 1. Understandable Advanced Mathematics by Didas.<br>2. Advanced Mathematics by CHAND<br>3. Advanced Mathematics TIE Form Five. |
| 4. | Geography | 1. Physical Geography<br>2. Practical Geography for A-level by TIE |
| 5. | Physics | 1. Physics kidato cha Tano na Sita TIE<br>2. Principle of physics class Xi and Xii by S.CHAND<br>3. A-Level physics by ROGER MUNCASTER |
| 6. | History | 1. Vitabu vya History kidato cha Tano TIE |
| 7. | Kiswahili | 1. Kiswahili Fasihi na Sarufi Mwandishi TIE Mtaala mpya<br>2. USHAIRI (Malenga wa ziwa kuu, Fumbo linaloendelea, Andamo Msafiri Safarini.)<br>3. RIWAYA(Dunia Uwanja wa fujo, Ua la Faraja, Mirathi ya Hatari, Wasifu wa Binti Saad)<br>4. TAMTHILIYA (Mkwawa wa Uhehe, Shijaa Mirambo, Usaliti Mjini) |
| 8. | English Language | 1. English language for Advanced Level Book by TIE<br>2. A taste of Heaven by Farouk Topan<br>3. The Government Inspector by Nikolai V. Gogol<br>4. Summons: Poems from Tanzania by Richard S Mabala.<br>5. The Horizon Unveiled by Fellowers Mwaisela.<br>6. Chasing the Leopard Finfind the Lion by Julie Wakeman-Linn<br>7. Opportunist Elite by Nyambari Nyangwine |
| 9. | Economics | 1. Microeconomics na Macro economics New Syllabus. TIE |
| 10. | Academic Communication | 1. Kidato cha TANO kutoka TIE<br>2. A Compendium of Academic Communication form five student's notes by Samson Mwita |
| 11. | Historia Ya Tanzania Na Maadili | 3. Kidato cha TANO kutoka TIE |

Kiambatisho: A

**TARIME SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Full Name ……………Age ……………… Height (in cm) …………………….. Weight (in kgs)……………

1. Blood count ……………………..(Red and White) …………………
2. Stool Examination…………………………………
3. Urine Analysis ……………………………………………
4. Syphilis and other V.D ………………………………
5. T.B and Leprosy Test………………………………………
6. Eye Test ……………………………………………………
7. Ear Test ………………………………………………………………
8. Chest Test……………………………………………………………
9. Abdominal Test…………………………………………………………
10. Blood Group (very crucial)…………………
11. Spleen ……………………………………………………………………
12. H.I.V Test, positive ……………………….. Negative …………………… (Tick where necessary)

Additional information e.g. physical defect or impairments, infections, chronic or family Diseases (e.g. sickle cell).

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………….

I certify that the above student is fit/is not fit to pursue secondary Education.

Signature ……………………………………………………….

Designation…………………………………………………….

Station………………………………………………………….

Date………………………………

PICHA PASSPORT SIZE YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI TARIME**

**Kiambatisho:B**

PICHA PASSPORT SIZE YA MWANAFUNZI

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye TSM 9/ Sel Form)……………………………………………

2. Anwani ya nyumbani ………………………………………………………………………..

3. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………... (***Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa siku ya kuripoti***)

4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji……………………… Kata……………………… Tarafa……………… Wilaya…………

5. Mahali unapoishi kwa sasa . Kijiji……………………… Kata……………………… Tarafa……………… Wilaya……

6. Shule ya Sekondari uliyomalizia………………………………………Anwani………….………………………

7.Dini/Dhehebu……………………………8.Kabila……………………………………………………

9.Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania……………………………………………..

**10. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala yahusuyo shule (Ni lazima kujaza sehemu zote nne)**

i) Jina la Baba………………………………………… Namba ya Simu …………………

Anaishi/Haishi……………………………… Kazi yake ………………………………… Anwani………………………

**ii) Jina la Mama**……………………………………………… Namba ya Simu …………………

Anaishi/ Haishi……………………………………… Kazi yake ……………………..…… Anwani…………

**iii) Jina la Mlezi (1)**……………………………Uhusiano…………………… Namba ya Simu ………….

Kazi yake …………………………………………………………………………………………

Anwani…………………………………………………………………………………………….

**iv) Jina la Mlezi (2)**…………………………… Uhusiano…………………… Namba ya Simu ………… Kazi yake ………………………………Anwani……………………………………………..………

Mimi (**Mwanafunzi**)……………………………………………………….. nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninahaidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

Jina kamili la Mwanafunzi ……………..………………. Sahihi ya Mwanafunzi………………Tarehe …………..

Mimi (***Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi***)…………………………………………………ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi …………………………………nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari TARIME ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Nahaidi kwamba nitamuhimiza mwanagu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha nahaidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanagu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

Jina kamili la Mzazi/mlezi ……………..………………. Sahihi ya Mzazi/mlezi ……………Tarehe …………..

**KIAMBATISHO: C**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI TARIME**

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Ikiwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wamekubaliana na masharti yote ya shule, sharti fomu hii isainiwe na watu wanne, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe: Jina kamili……………Kidato……..Tahasusi……………Saini…………Tarehe……

(ii) Mzazi/Mlezi: Jina kamili…..............................Namba ya Simu………..…Saini ……………Tarehe……………

(iii) Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa: Jina la Kijiji/Mtaa …………………… Wilaya……………… Mkoa…………

Jina la Afisa Mtaa/Kijiji:………………………………………………………..

Maoni/Mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu:
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------ -------
-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------ -------
------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Saini ya Afisa Mtendaji ________________________________ Tarehe _______________

Mhuri wa Afisa Mtendaji:

Namba ya simu_________________________________________